

HALMASHAURI YA WILAYA YA MASWA
(Barua zote zitumwe kwa Mkurugenzi Mtendaji Wilaya ya Maswa)

Telegrams: "MSW"
Telephone: +028 2750271
Fax: +028 2750376
E-mail: ded@maswade.go.tz



S.L.P 170,
MASWA,
SIMIYU.

Kumb.Na. MDC/ADM/10/30/VOL 1/88

26 Mei, 2022

YAH: TANGAZO LA NAFASI YA KAZI

Halmashauri ya Wilaya ya Maswa imepata idhini ya kutekeleza ikama na Bajeti kwa mwaka wa fedha 2021/2022, kupitia barua **Kumb. Na.FA.97/288/01/09** ya tarehe **13/05/2022**, iliyotolewa na Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Maswa anatangaza nafasi za kazi ya **Mtendaji Daraja la III** kwa Masharti ya kudumu, hivyo Watanzania wote wenye sifa hizo mnakaribishwa kutuma maombi ya kujaza nafasi hizo kama ifuatavyo:-

1.0 MTENDAJI WA KIJIKI DARAJA LA III – NAFASI 12

1.1. Sifa za Mwombaji:-

- i. Wahitimu wa kidato cha nne au sita wenye cheti cha [NTA Level 5] au Certificate katika moja ya fani zifuatazo.
- ii. Utawala
- iii. Usimamizi wa Rasilmali watu
- iv. Maendeleo ya Jamii, Sheria, Usimamizi wa Fedha au
- v. Sayansi ya Jamii kutoka Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo, Dodoma au chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali
- vi. Awe na umri usiozidi miaka 45
- vii. Awe na cheti cha kuzaliwa.

1.2. MAJUKUMU YA KAZI

- (i) Afisa Masuuli na Mtendaji Mkuu wa Serikali ya kijiji,
- (ii) Kusimamia Ulinzi na Usalama wa Raia na Mali zao, kuwa mlinzi wa Amani na Msimamizi wa Utawala bora katika kijiji.
- (iii) Kuratibu na kusimamia upangaji wa utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo ya Kijiji.
- (iv) Katibu wa Mikutano na Kamati zote za Halmashauri ya Kijiji.
- (v) Kutafasiri na kusimamia Sera, Sheria na Taratibu.
- (vi) Kuandaa taarifa za Utekelezaji wa kazi katika eneo lake na kuhamasisha wananchi katika kuandaa na kutekeleza mikakati ya kuondoa njaa, umaskini na kuongeza uzalishaji Mali.

- (vii) Kiongozi wa Wakuu wa vitengo vya Kitaalam katika Kijiji.
- (viii) Kusimamia, kukusanya na kuhifadhi kumbukumbu zote na nyaraka za Kijiji.
- (ix) Mwenyekiti wa kikao cha Wataalamu walilopo katika Kijiji.
- (x) Kupokea, kusikiliza na kutatua malalamiko na Migogoro ya Wananchi.
- (xi) Kusimamia utungaji wa Sheria ndogo za Kijiji.
- (xii) Atawajibika kwa Mtendaji wa Kata.
- (xiii) Kazi nyingine utakazopangiwa na Mwajiri.

1.3 NGAZI YA MSHAHARA

Mshahara: Ngazi ya **TGS B** kwa mwezi.

3.0. MASHARTI YA JUMLA

- Awe raia wa Tanzania.
- Awe na umri wa kuanzia miaka 18 hadi 45
- Waombaji waambatanishe nakala za cheti cha kuzaliwa, vyeti vya kuhitimu mafunzo na vyeti vya kidato cha nne vilivyothibitishwa na Wakili au Mahakama.
- Muombaji ambatanishe picha mbili [2] ndogo ya rangi [passport size] ya hivi karibuni.
- Testimonials, Provisional results, Statement of results na hati za matokeo ya kidato cha nne na sita [form VI and form IV result slip] **HAVITAKUBALIWA.**
- Waombaji ambao wapo kwenye Ajira, barua za maombi zithibitishwe na Waajiri wao.
- Waombaji waliostaafishwa katika Utumishi wa Umma hawaruhusiwi kuomba isipokuwa kwa Kibali cha Katibu Mkuu Kiongozi.

4.0. UTARATIBU WA KUTUMA MAOMBI


Maombi yote yatamwe kwa:-

Mkurugenzi Mtendaji (W),
Halmashauri ya wilaya ya Maswa,
S.L.P. 170,
MASWA –SIMIYU.

Mwisho wa kupokea maombi ni **tarehe 10.06.2022 Saa 9.30 Alasiri.**

NB:

Tangazo hili linapatikana katika Tovuti ya Halmashauri www.maswadc.go.tz Tovuti ya Sekretarieti ya Ajira www.ajira.go.tz na katika mbao za mataangazo za Halmashauri na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Simiyu.


Simon Berege
**MKURUGENZI MTENDAJI (W)
HALMASHAURI YA WILAYA
MASWA**